# Madereva watakiwa kuondoa milio ya kelele kwenye pikipiki

Na Veronica Mheta, Arusha

MKUU wa Mkoa wa Arusha, Kenani Kihongosi ametoa siku tatu kwa madereva wa vyombo vya usafiri maarufu kama *bodaboda* kuondoa milio kama bomu waliyofunga kwenye pikipiki zao ambayo yana kelele za kushtua na kusababisha kero kwa wananchi pamoja na watumiaji wa usafiri huo.

Kihongosi alitoa rai hiyo juzi baada ya kujadiliana na madereva hao kuhusu kero hiyo inayolalamikiwa na wakazi na watumiaji wa vyombo hivyo vya usafiri kwenye maeneo yote ya mkoa huo, wakati wa kikao cha madereva wa bodaboda, bajaji na maguta kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid mkoani Arusha.

"Nimeletewa kero hii na wazee na viongozi wetu wa dini, unapopiga fataki hiyo kumbuka kelele hizo zinaleta kero kubwa kwa watu wanaosikia, kuna wagonjwa, kuna wazee na wengine wenye shida nyingine, fanyeni utaratibu wa kuondoa kifaa hicho kinachotoa kelele yenye kero, hivyo natoa siku tatu kama mlivyokubaliana hapa," alisema.

Hata hivyo aliwataka madereva hao kuheshimu na kuithamini kazi hiyo na kuhakikisha wanaendesha vyombo hivyo vya moto kwa kuzingatia sheria na taratibu pamoja na kutumia fedha hizo kwa ajili ya maendeleo.

"Tumieni kazi yenu kuwaletea maendeleo ya kiuchumi na kijamii, tumieni fedha vizuri kwa kuwa na malengo ya kimaendeleo lakini nyie 'tatu mzuka' mnaowaibia wananchi na watu mbalimbali acheni hiyo tabia ukikamatwa hutoki," alisema.

Awali, Katibu wa Maofisa Usafirishaji Mkoa wa Arusha, Hakimu Msemo alisema wanatamani kila dereva wa bodaboda awe anatambulika kwenye mfumo wa kidijiti ambapo wanachama 8,000 wamesajiliwa na kujulikana kwa haraka endapo amepata changamoto ikiwemo sare.

Msemo alisema umoja huo umeimarisha uongozi kwa kata 25 ikiwemo usajili huo kati ya vituo 511 vilivyopo jijini hapa ambapo mfumo huo unaweza kuwa na wanachama zaidi ya 200,000 lakini pia wana ndoto ya kuanzisha ushirika ambapo mpaka sasa wana jumla ya Sh milioni 23 ambazo zipo ndani ya ushirika wao unaotarajia kuanza.

Alisema Sh milioni 10 walipewa na Rais Samia Hassan Suluhu, ambapo kwa sasa wanaunganisha wanachama na taasisi mbalimbali ikiwemo kushirikiana na jeshi la polisi katika kuimarisha ulinzi na usalama.

Scanned with CamScanner